# *Hisi Kuu*

Ningali ninafurahia, pia, baraka hiyo asubuhi ya leo.

Loo, mambo mengi, yaliyozidi sana, huwezi kujua, mambo ambayo Mungu angetufanyia tunapokusanyika pamoja! Je! umetambua tangu tulipojiweka wakfu kwa Mungu, jinsi ambavyo mambo yamekuwa yakiendelea hapa? Baraka baada ya baraka, nguvu baada ya nguvu, utukufu baada ya utukufu! Limekuwa ni jambo la ajabu kabisa. Naye ataendelea kufanya hivyo. Leso hizi, nimeziombea, ambazo—ambazo ni za mtu fulani hapa.

2 Sasa nataka kutamka machache, kwa dakika moja ama mbili, na kwanza kuwashukuru ninyi nyote kwa zawadi yenu nzuri ya Krismasi, ya ile suti mliyoninunulia. Hiyo ndiyo iliyokuwa katika chako, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Naam, bwana. Naam, bwana."—Mh.] Naam, bwana. Naam, suti. Mbona, wahubiri sikuzote wanaweza kutumia suti. ["Inanienea vizuri kabisa."] Nzuri sana! Hilo ni jambo zuri. Sasa, wao hutokwa na jasho, na jasho hilo huozesha nguo upesi kuliko kitu cho chote ninachojua, unaona. Na inahitaji nguo nyingi sana kumtosheleza mhubiri, na nguo nzuri. Kitambaa rahisi sana cha pamba kitaoza kabisa, katika muda mfupi tu. Kwa hiyo su—suti nzuri kama hiyo kidogo itadumu muda mrefu.

3 Na hebu wazieni tu, mnawasaidia na kuwapa nguo hizi watumishi wa Bwana. Na Bwana awabariki. Yesu alisema, "Kadiri mlivyowatendea walio wadogo sana wa hawa ndugu zangu, mmenitendea Mimi." Kwa hiyo basi kamwe hamkuwaletea, hamkuwanunulia wahudumu wawili suti; mmemnunulia Yesu suti mbili. A-ha. Hivyo ndivyo alivyosema, "Mmenitendea Mimi."

4 Lakini mguso huo mdogo wa Kimbinguni, asubuhi ya leo, mliutambua? Hakuna mwaliko wa madhabahuni, hakuna kitu cho chote; lakini baada tu ya huo Ujumbe na—na burudisho la Roho Mtakatifu akiwalowesha watu, utukufu wa Mungu ukitenda kazi, wanaanza tu kuja, na kushuka, kila mahali. Nami niliwaona marafiki wangu wa thamani kweli kweli wa Kibatisti, kutoka Kanisa la Kibatisti la Barabara ya Walnut, huko Louisville, wamesimama kwenye marefu ya kanisa, wakioga tu katika nguvu za Mungu. Loo, jamani! Nami nilikutana nao baada ya ibada, wakasema, "Hizo ni nguvu za Mungu."

Nikasema, "Hiyo ni kweli...Mmesema kweli, bila shaka mmesema kweli. Nguvu za Mungu!"

5 Nawe huwezi tu kupata maneno ya kutamka. Mtu hata hajui la kusema. Roho Mtakatifu anauteka nyara tu mkutano nawe hujui atakalofanya nao. Kimya, kwa utamu, unyenyekevu, kwa

kuvunjika. Loo, Ndugu Pat, hilo ni Mbinguni tu, kwangu mimi. Mimi ni mmoja tu wa hawa wa mtindo wa kale wanaopenda kule kujihisi ndani Yake, unaona.

6 Kama yule hayati Paul Rader, alimwambia nanii wake... Wakati mmoja alikuwa akisimulia hadithi fulani. Naye akasema yeye na mke wake walikuwa wameketi mezani, na mke alitaka kwenda mahali fulani ama kufanya jambo fulani, naye kila mara alimwambia, "Siwezi kufanya hivyo kamwe," na kadhalika, naye angemkatiza maneno kidogo.

7 Kwa hiyo akamwangalia mke, na machozi yalikuwa yakitiririka shavuni mwa mkewe, ndipo akamwambia, akasema, "Vema, sasa," akawazia moyoni mwake, "kama yeye anaumia kwa urahisi jinsi hiyo, basi na aendelee kuumia." Kwa hiyo yeye, kama ilivyo wanaume, alikunja karatasi yake na kuiweka juu ya sahani yake.

8 Na huyo mama sikuzote alisimama mlangoni na kumbusu kwa heri; ndipo wakati alipotoka nje ya lango, mkewe angempungia mkono, na basi jambo hilo linge—hilo lingetosheleza, unajua, mpaka aliporudi kutoka ofisini kwake.

9 Na kwa hiyo asubuhi hiyo, kasema, walipoanza kwenda, mbona, ninii...pale mlangoni, mbona, huyo mama alikuwa amesimama mlangoni, naye akambusu mkewe kisha akaenda mpaka mwisho wa lango, akafungua lango na kuangalia nyuma, naye mama huyo alikuwa amesimama mlangoni ameinamisha kichwa chake, angali ameumia, kasema alimpungia mkono kumuaga, akasema mama naye akampungia mkono kumuaga.

10 Kasema alianza kwenda zake barabarani, ndipo akaanza kuwazia, "Vipi kama jambo fulani lingenipata kabla sijafika nyumbani, ama, vipi kama jambo fulani lingempata kabla sijarudi, Mungu angetuita tukaaga dunia; na jinsi alivyokuwa mwanamke mzuri, na jinsi alivyokuwa ni mwenye upendo, na kadhalika?" Ndipo akasema, kadiri alivyoenda mbali, ndivyo moyo wake ulivyoanza kujaa.

11 Kwa hiyo aligeuka tu akarudi mbio, akafungua lango, akakimbia ndani ya nyumba, akafungua mlango. Na alipofungua mlango, akasikia kitu fulani kikilia. Akaangalia kote, huyo mama alikuwa amesimama nyuma ya mlango. Kasema hakusema kamwe "nisamehe," hakusema kamwe "naomba radhi," hakusema kitu. Kasema alimkumbatia tu na kumbusu tena, akageuka na kutoka. Kasema alitoka nje ya lango, kasema huyo mama alikuwa tena amesimama mlangoni. Akasema, "Kwa heri." Na mke akasema "Kwa heri," kasema, kama vile tu alivyofanya mara ya kwanza, lakini hii mara ya mwisho ilikuwa na kujihisi moyoni.

12 Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Wakati jambo lina kujisikia moyoni, unaona, ya kwamba kweli ni jambo fulani kutoka kwa Mungu.

13 Sasa katika kule kuchaguliwa dakika chache zilizopita, kwa mdhamini mpya, Ndugu Sothmann. Nina hakika ya kwamba wadhamini, na hao wote, wanajua sasa, ya kwamba, mwisho wa mwaka wa fedha, mnamo Januari moja, kwamba huduma zote za kanisa, kama vile wachungaji na mashemasi, na kadhalika, zamu huisha. Ndipo kama wao wanataka kuendelea... Si wachungaji; sikumaanisha hao. Nilimaanisha wadhamini, na mashemasi, na waalimu wa shule ya Jumapili, na kadhalika. Kwamba, mchungaji anachaguliwa na kanisa, naye anakaa mpaka, mpaka. Halafu— halafu wao...Kama hao watu, halmashauri iliyopo sasa ya wadhamini, ama mashemasi, ama waalimu wa shule ya Jumapili, ama wo wote wale, kama wanataka kuendelea, wanaendelea tu. Kama hawataki, basi hawana—hawana budi kujiuzulu kama hawataki kuendelea; wala hakuna neno dhidi yao. Basi wataendelea kwa mwaka ujao. Ndipo—ndipo basi endapo hawaendelei, basi wanafanya uchaguzi, na kuwachagua wadhamini wengine, ama—ama ikiwa ilikuwa ni ofisi yo yote ile.

14 Kwa hiyo, haimfungi mtu, maishani mwake, kutumika katika halmashauri. Lakini mradi tu anajisikia ya kwamba Mungu yuko pamoja naye na anamsaidia, naye anataka kutimiza jukumu lake, ama yeye mwanamke kutimiza jukumu lake, cho chote kile ingelikuwa, kuendeleza kazi ya Mungu, daima tuna furaha kutumika pamoja nao. Unaona? Lakini kwa njia hiyo inampa mtu nafasi ya kutumika kwa mwaka mmoja na kuona jinsi wanavyolipenda jambo hilo. Baadhi ya wadhamini wetu huendelea kukaa kwa miaka kadha wa kadha, na mashemasi pia, na hilo ni sawa kabisa. Lakini basi hakuna wakati uliowekwa maalum. Kama mdhamini, ama mchungaji, ama mtu fulani kwenye halmashauri, hajisikii kama anaweza kuendelelea kutumika zaidi, ama anahama, basi wanaliarifu tu kanisa, kusudi wapate kuweka mtu wa kuchukua mahali pao.

15 Na jambo hilo ndilo lililotukia hapa usiku wa leo, na Ndugu Morgan, kujiuzulu kwa Ndugu William Morgan kama mdhamini. Walihitaji mdhamini mwingine. Na Ndugu Sothmann alichaguliwa kuwa mdhamini, katika kipindi kingine, na ndipo usiku wa leo akapokelewa kwenye halmashauri.

16 Ni jambo rasmi, kulingana na kanisa. Katika kanisa letu, kanisa ndilo lenye mamlaka. Kanisa huondoa, ama kuingiza wadhamini, kanisa humwondoa mchungaji, ama linamweka mchungaji, cho chote kile, ni kanisa katika kila jambo. Huko ni kuenenda kimitume. Hivyo ndivyo ilivyofanyika katika wakati wa Biblia. Kwa hiyo, tunajisikia ya kwamba hakuna mtu mmoja peke yake, basi, ni kiongozi wa mabavu ama cho chote kile kanisani. Hatutaki jambo hilo. Kila mwanamume, kila mtu, mimi mwenyewe, katika kumchagua mtu ye yote, ana kura moja tu, kama mtu ye yote tu yule wa kanisa hapa, kura moja tu. Si kile ninachosema; ni vile kanisa linavyosema, unaona, vile

kanisa linavyosema katika ule mwili. Mnapenda jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, nafikiri hilo ni la Kimaandiko kabisa. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

17 Sasa, hili litakuwa ni juma muhimu sana kwangu, lijalo, kesho, Bwana akipenda. Sina budi kufanya maamuzi kwa ajili ya mwaka ujao, juu ya mialiko yote. Nataka kwenda o—ofisini na kuchukua mialiko yangu yote na kuileta nyumbani. Na kwa hiyo, kwa siku chache zijazo, nitaingia katika maombi, kwa Mungu, nimwombe kwamba Yeye aniongoze na kuinionesha kwamba niendee njia gani na nifanye nini. Hatuishi katika wakati kama ulivyokuwa wakati Yeye alipokuwa hapa, ambapo Mungu alimwongoza toka mahali hadi mahali, Naye alikuwa mjini kwa masaa machache kisha ameondoka ameenda kwenye mji mwingine. Bali siku hizi liko kwenye utaratibu mwingine, hali ndivyo ilivyo, makundi ya wahudumu na mambo chungu nzima hayana budi kushughulikiwa.

18 Na jinsi ninavyolifanya, ninaleta mialiko yangu yote ya Afrika na kuiweka chini, mialiko yote ya India, na yote ya California yote, Utah, na mialiko yote mbalimbali, na kuitenganisha katika mafungu mbali mbali. Nitaiacha ikae hapo. Ndipo ninaanza kutembeatembea na kuomba, labda niingie kwenye gari langu na nisafiri niende zangu kwa siku moja ama mbili. Nirudi, nikiomba. Jambo fulani linaingia moyoni mwangu kuenda mahali fulani, ndipo ninachunguza nione kama ni wazo tu. Halafu, baadaye, ndipo ni. . .kama limenisukuma sana, ninaenda kwenye lundo hili lililo na mahali hapo, ndipo ninachukua barua na kuisoma, ya mwaliko, kuona kwamba ni wapi. Halafu, kutoka hapo.

19 Sababu ya mimi kufanya jambo hilo ni hii. Hebu wazia juu ya kusafiri kwa ndege saa sabini na mbili, katika matufani, na kwenda juu na kushuka chini, na huku na huko, kama ulipata kusafiri nchi za ng'ambo. Wakati mwingine hujui kama mko—mko juu, na wakati mwingine mnashuka, na huku mnabembea, na kuyumbayumba, na kuvurumishwa, katika hayo mawingu na juu ya hayo maji, kwa muda wa siku mbili usiku na mchana. Ndipo unaingia kwenye nchi fulani, na kitu cha kwanza kinachokukabili ni Shetani, "Vema, kundi la wahudumu lilisema *hivi*, baadhi yao wamegawanyika katika kura, na wengine wanaunga mkono." Unaona?

20 Ndipo huenda ukasema hivi, "Vema, labda Bwana hakutaka nije."

21 Lakini wakati unapotumwa na Mungu, uko tayari kukutana na adui. Unasema, "Ninakanyaga hapa, katika Jina la Yesu Kristo. Nimekuja katika Jina la Bwana Yesu, na nitakaa hapa mpaka kazi Yake itakapomalizika." Unaona, ndipo uko tayari kukabiliana na majeshi.

22 Kwa hiyo, mnanipenda, ninajua mnanipenda. Kwa hiyo niombeeni juma hili, nipate kufanya maamuzi mazuri, kwa kuongozwa na upako wa Mungu.

23 Sasa nitakuwa na mikutano midogo michache, ninayoita, mikutano ya kurukaruka. Ninashuka kwenda Florida, tarehe nane, tisa na kumi ya mwezi huu; ama, Tifton, Georgia. Tifton, Georgia, tarehe nane, tisa na kumi Januari, ndivyo nilivyomaanisha kusema, badala ya mwezi huu. Na ndipo sina budi kwenda Glasgow, Kentucky; na labda Somerset, Kentucky; na usiku mmoja, na labda Campbellsville, Kentucky. Na— na Ndugu Rogers alinitaka nije kwa usiku mmoja, nyumbani kwake, ambapo tulipata . . . tulilazimika kumkosa wakati ule uliopita.

24 Sasa, mwombeeni Ndugu Rogers. Tulikuwa na ushirika, leo, nami nikashika mkono wake nikamkuta yuko katika hali mbaya, kimwili. Kwa hiyo mwombeeni Ndugu Rogers ambaye yuko hapa. Amechukua mambo mengi mkononi mwake kule aliko, na jambo hilo limemfanya kuwa na wasiwasi na kuhangaika, naye ana—ana afya mbaya sana sasa hivi, na mke wake ni mahututi. Kwa hiyo mwombeeni maskini huyo mtu na mkewe, watoto wazuri wa Mungu. Nami nilimwambia ya kwamba, Bwana akipenda, nitampa usiku mmoja.

25 Na Ndugu Rudell, maskini maninii yetu madogo . . . moja ya makanisa yetu shirika, hapa kwenye 62, maskini mvulana mdogo mwenye soni, alitembea hapa na hata asingeweza kuangalia juu. Naye angekuja nyumbani. Na, loo, nafikiri watu walifikiri yeye alikuwa ni kero kabisa, bali kulikuwa na jambo fulani kwa mvulana huyo lililoonekana halisi. Niliendelea tu kukaa naye, na kukaa naye, niseme "Ndugu Ruddell, unaweza."

26 Akasema, "Ndugu Branham, ninasimama mbele ya umati wa watu, moyo wa—wangu unapanda kwenye koo langu, na— na— nami siwezi kusema neno hata moja."

27 Nikasema, "Simama hapo na uumeze moja kwa moja, na useme, katika Jina la Bwana, unaona." Na sasa ana Maskani ukubwa wa hii, hapa kwenye barabara kuu, akifanya jambo fulani kwa hakika. Kaa na jambo. Mvulana huyo alikuwa na wito wa Mungu. Nilimjua baba yake na mama yake, ni watu wazuri sana.

28 Na tena tunapaswa kuwa na Junie, usiku mmoja, kule New Albany. Na, loo, unajua, mikutano midogo midogo tu, ambayo naweza kupata usiku mmoja hapa na usiku mwingine pale.

29 Mpaka, kama kila kitu kikienda kulingana na ratiba, mnamo tarehe ishirini na tano Januari, nitaondoka kwenda Miami, kwa ajili ya Mkutano wa Kimataifa wa Wafanyi Biashara wa Injili Yote Ulimwenguni. Na kutoka hapo, niende Kingston, Haiti, nishuke niende Amerika ya Kusini, na nipande kupitia Mexico. Na kutoka huko, niingie Afrika. Kutoka Afrika, niende

mpaka nchi za Skandinavia. Na kadhalika, namna hiyo. Sehemu kubwa sana ya mwaka, ninaamini, itaishia katika mikutano ya nchi za ng'ambo. Kwa hiyo niombeeni, sina budi kufanya maamuzi sahihi.

30 Sasa hiyo ni kama tu itakuwa ni mapenzi ya Bwana; kama siyo, niko tayari kwenda mahali po pote, sehemu yo yote. Haidhuru ni wapi, ninataka kwenda. Lakini mradi tu ninaweza kusimama katika mavumbi haya ya nchi mahali ambapo Mungu ameniweka, ninataka kuhubiri utajiri wake usiopimika mpaka mauti itakaponiondoa mahali hapa. Hilo ndilo azimio langu, kwa neema ya Mungu, kama tu Yeye atanisaidia. Kama akiondoa mkono Wake kutoka kwangu, ibilisi ataniua, kwa hiyo ombeni tu ya kwamba Mungu ataweka mkono Wake wa rehema juu yangu.

31 Siombi haki Yake; ninaomba rehema Yake. Unaona? Sasa, haki Yake, la, nisingeweza kustahimili hiyo. Ninasihi tu nipate rehema Yake, maana ninajua mimi sistahili, wala hakuna mtu anayestahili. Na afadhali tusiombe haki Yake. Tunataka rehema Yake.

32 Sasa, usiku wa leo, nikiwa nimepwelewa na sauti kidogo, bali singeweza kutupa nafasi hii, kuzungumza na kundi hili zuri la Wakristo. Ngoja, kabla tu ya mimi kutoa tangazo hili, hebu niseme jambo moja. Wakati nyote mkiwa katika moyo mmoja sasa, katika umoja, na kila kitu kikiendelea vizuri, hebu nizungumzie kanisa langu kwa dakika mbili, unaona.

33 Sikilizeni, wapendwa wangu katika Injili, ninii yangu... nyota katika taji langu, kama nitapata moja, ninyi mlionunuliwa kwa Damu ya Yesu. Nilifanya jambo hili kwa kusudi fulani, kurudi namna hii. Tuliamua jambo hilo kwenye safari ya kuwinda, Ndugu Roy Roberson, Ndugu Banks Wood, pamoja na mimi, kwenye safari fulani, ya kwamba tungeweza kuleta, tungerudi. Ndugu—Ndugu Roy na sisi sote tulikuwa tukizungumza, na juu ya mchungaji wetu, Ndugu Neville, na mtu aliye mbele zenu wakati wote, akiwachunga na kadhalika, tunampenda; lakini hata hivyo, Ndugu Neville akiwa msaidizi wa mchungaji, imeonekana kidogo ni vigumu kwa Ndugu Neville kulazimika kujisukumiza katika jambo hilo, unaona. Kwa hiyo tuliomba, na ilielekea kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Bwana kwamba nifanye jambo hilo. Sasa, nilimwomba Bwana kama angenisaidia, ningefanya vizuri niwezavyo.

34 Na baada ya kujiweka wakfu mimi mwenyewe, na baada ya kufanya ninii, kulifanya kanisa lijiweke wakfu sasa, kama Mungu alitubariki sisi jinsi alivyofanya katika mikutano michache iliyopita, na huko kujiweka wakfu kudogo, Je! Yeye atafanya nini kama tukishikilia jambo hilo, unaona? Kuendelea kulidumisha tu. Sasa sikilizeni. Ninyi mnapendana, jinsi ninavyowaona mmesimama kwenye marefu ya kanisa,

asubuhi ya leo, na kulia tu, huku mmemwinulia Mungu mikono yenu, na—na Roho wa kupendeza akipitia juu yenu.

35 Sasa msisikilize hata jambo moja baya ibilisi analotaka kusema. Mnaona? Kama ibilisi akiwaonesheni baadhi yake, ama akiwaambia jambo baya, juu ya mmoja wa washiriki wa Mwili wa Kristo, msiliamini. Kwa maana, mara mkiliamini, mnaharibu ushuhuda wenu.

36 Na kama ukiona mmoja wa washiriki wa Mwili wa Kristo akifanya jambo fulani baya, usimwambie mtu mwingine; bali mwendee mshiriki huyo, na kwa upendo, na uone kama huwezi kuwarudisha kwa Kristo tena. Na kama huwezi kufanya jambo hilo, basi mwambie mtu mmoja, ama chukua watu waende pamoja nawe. Fanya jambo hilo jinsi Maandiko yalivyosema. Unaona? Lakini usininii . . .

37 Kama mtu fulani akisema, "Dada *Fulani*, ama Ndugu *Fulani*," usiamini hata neno moja kuhusu jambo hilo. Liachilie mbali kabisa. Kwa maana, kumbukeni, ni ibilisi akijaribu kuwararua vipande-vipande. Sasa mtazamieni aje, maana atafanya jambo hilo. Sasa mwache mkazi mwema wa nyumba, imani, asimame mara moja pale, wala usipokee hata jambo moja. Watu hawa wamewekwa katika ulimwengu wa roho pamoja na wewe, kushiriki pamoja katika baraka za Mungu, wakishiriki Meza ya Bwana, na Roho Mtakatifu ameshuhudia ya kwamba wao ni wana wa Mungu. Hebu na tuwe wapole sana, wenye huruma, wenye kusamehe, wenye kupenda. Na kama mtu huyo mwingine akinena mabaya dhidi yako, wewe nena mema juu yao. Angalia basi jinsi mnavyozidi kuwa wenye upendo. Unaona? Hiyo ni kweli. Hebu sikuzote rudisha wema kwa ubaya, upendo kwa chuki. Na uninii tu . . .

38 Je! unajisikia nafuu zaidi, kipenzi, yule msichana mdogo kule nyuma? Hilo ni sawa. Ninashukuru sana. Naam, ndio kwanza tu arudi . . . Alikuwa amekunjwa nyuma kule katika kifundo, na Bwana Yesu amemwinua sasa na kumleta mkutanoni. Tunashukuru sana kwa jambo hilo. Hicho ndicho kilichosababisha nikaondoka mimbarani, muda mchache uliopita. Walisema walikuwa "wameomba na kuomba, hawangeweza kupata jibu kwa Bwana."

39 Sasa, hakikisheni mtafanya jambo hilo. Jiwekeeni nadhiri juu ya jambo hilo, kwa Mungu, "Mungu, kwa neema Yako, hivyo ndivyo nitakavyofanya." Haidhuru wakati mtu ye yote anaponena jambo baya; nirudishe mema. Usiwazie uovu. Kama unawazia uovu, nawe unasema tu jambo hilo kinafiki, basi—basi—basi uko makosani. Endelea tu kujitakasa kwa Mungu mpaka utakapojisikia kumpenda mtu huyo. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Ndipo utamu wa baraka za Mungu utaninii tu, loo, utafunika tu nafsi yako. Hiyo ndiyo jinsi ya kuishi kwa

ushindi, ndipo hakuna kitu kinachoweza kukudhuru mradi tu wewe unampenda sana mwingine. Vema, unasema . . .

40 Unaona, "Kama mna kunena kwa lugha, kutakoma. Na kama mna hekima, itakwisha. Unabii, utakoma. Bali ukiwa na upendo, utadumu milele." Unaona?

41 Wala msiwapende tu hao wanaowapenda ninyi, bali wapendeni hao wasiowapenda. Kwa kuwa, ni rahisi kwangu kumpenda mtu ye yote anayenipenda, lakini jaribu kumpenda mtu asiyekupenda. Hapo ndipo unapoweza kupima kama wewe ni Mkristo ama la; mtu fulani ambaye hakupendi, na hata hivyo, moyoni mwako, unawapenda. Sasa, kama hufanyi jambo hilo, basi endelea tu kumshikilia Mungu. Lipo, maana ninajua hilo ni Kweli. Amina. Ninajua kwamba jambo hilo ni Kweli.

42 Sasa tutafungua Neno la thamani, sasa, kwenye Kitabu cha Waebrania, na mlango wa 11, kwa Ujumbe mfupi tu.

Kwa kuwa nimepwelewa kidogo na sauti, lakini nilikuwa na alasiri ya furaha sana nikiwa pamoja na ndugu na dada. Na sikurudi nyumbani mpaka karibu thenashara, na ndipo nilikimbilia tu chumbani na kupiga magoti kando ya kitanda, katika chumba cha kulala, na kuomba kwa dakika chache. Nikaamka, nikachukua Biblia yangu na kuanza kusoma. Ndipo nikaona gazeti limewekwa pale, nami nikalichukua, nalo lilikuwa limeandikwa katika Kiafrikana, kwa hiyo sikuweza kulisoma.

43 Na mara nyingi, katika kusoma, utaguswa na neno, na neno hilo linahuika kwako. Hivyo ndivyo ambavyo mhudumu anavyopata ninii yake, ujumbe wake. Anza tu kusoma, kusoma Biblia, kitu fulani. Muda si muda unajua, unaguswa na kitu fulani, kisha jambo lingine linaongezeka kwenye jambo hilo, jambo fulani linaongezeka kwenye hilo jambo fulani. Basi, lipigie mstari, na uende tu mimbarani na kulisoma. Mungu atafanya hayo yaliyosalia. Unaona, Yeye atashughulikia hayo mengine.

44 Sasa, mara nyingi na unazama kiasi kwamba, mpaka unaandika mawazo madogo ya ninii, maneno machache juu ya mawazo ambayo umeyawazia. Mara nyingi katika mkutano, ambapo huna budi kuja upesi jukwaani, ambapo, hebu soma tu hayo mawazo madogo uliyokuwa nayo, labda Roho Mtakatifu atayahuisha kwako tena. Nimefanya hivyo mara nyingi.

45 Sasa Waebrania 11, hebu tusome kifungu cha 1, mwanzoni, nasi tutasoma vifungu vichache.

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*
>
> *Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.*

*Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*

46 Hilo si ni tamu mno? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu nisome hicho kifungu cha 3 tena. Sikilizeni kwa makini.

*Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.* (Ni Neno la Mungu!)

*Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki, Mungu akazishuhudia sadaka zake: na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena!*

*Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.* (Miaka mia tano ya maisha, pia!)

*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.*

*Kwa imani Nuhu, akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. . .hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo—ipatikanayo kwa imani.*

47 Sasa hebu kidogo tuombe, na tuinamishe vichwa vyetu.

48 Bwana, Mungu wetu Mwenye Rehema Nyingi Sana na uliye Baba yetu, tunakuja sasa katika Uwepo Wako tena, tukiwa na shukrani. Na si kwamba tu tunajisikia ya kwamba tuko katika Uwepo Wako kwa sababu tumeinamisha vichwa vyetu kuomba, bali tunaamini ya kwamba daima tuko katika Uwepo Wako, kwa sababu kwamba, "Macho ya Bwana yapiga mbio huko na huko duniani mwote." Nawe unajua mambo yote, Nawe unajua mawazo ya moyo.

49 Kwa hiyo, Bwana, sababu ya sisi kuinamisha vichwa vyetu, ni kukuomba ombi hili, ya kwamba utusamehe kwa makosa yetu yote na dhambi zetu dhidi Yako, na kwamba rehema Zako mara nyingine tena zitakuja juu yetu, hata upate kufungua vinywa vyetu kunena na masikio yetu kusikia, na kwamba Neno Lako liweze kuwa halisi kwetu, usiku wa leo; ili kwamba vifungu hivi vichache ambavyo tumechagua kuvisoma vipate kuwa msaada mkubwa kwa kila mshirika wa mwili Wako wa kisiri duniani, Kanisa Lako la kiroho, Kanisa la Mzaliwa wa

Kwanza, lile Kanisa ambalo limenunuliwa na Damu ya Yesu, ambalo limeoshwa na limekwisha kutakaswa, na litatolewa kwa Mungu kwenye Siku ile, bila waa ama kunyanzi. Jinsi tunavyokushukuru, kuwa na imani kuamini ya kwamba sisi ni washiriki wa wema huu wa Mungu, kwa haki na rehema za Bwana wetu Yesu!

50 Naomba sasa ya kwamba utaponya magonjwa yote. Nakushukuru kwa kumgusa msichana yule mdogo dakika chache tu zilizopita, aliyekuwa amekunja chumbani kule, kutokana na maumivu; tukamwona akitoka nje, maskini imani hiyo iliyo kama ya mtoto mdogo, na kukukubali Wewe na rehema Zako. Na tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili; na naomba ya kwamba utamkumbuka mtoto mpendwa wa Dada Baker kule Kentucky, na wale ambao Ndugu Neville alizungumzia habari yao, na, Ee Mungu, kundi lisilohesabika la wagonjwa kila mahali. Na zaidi sana, Bwana, hao ambao hawajaokoka wala hawakujui Wewe; kama wakifa katika dhambi zao, wasingeweza kuja mahali ulipo Wewe.

51 Tunaomba ya kwamba utatupa ushuhuda pamoja na nguvu, ujasiri wa kulinena Neno, na hekima ya kujua wakati wa kulinena. Halafu nena nasi wakati tumesema ya kutosha, tupate kuondoka na kuwaacha watu katika mshangao, wakishangaa, juu ya Roho Mtakatifu aliye mkuu pamoja na kazi Yake. Tujalie, Bwana. Tusikie sasa, tunaomba, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

52 Nami ningetaka kuzungumza kwa muda mfupi tu juu ya somo la "hisi." Tunafundishwa ya kwamba mtu wa kawaida ana hisi tano, na hisi hizo tano zinatawala ninii ya— yake. . . Ama, Yeye alimpa, Mungu alimpa hisi hizi tano, apate kuwasiliana na makao yake ya duniani, na hisi hizo zinajulikana kama: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Hisi hizo tano zinazojulikana kwa mtu wa kawaida, nazo ni nzuri, wala hatuwezi kufanya kazi ama kuishi maisha ya kawaida wakati moja ya hisi hizi ikishindwa kutenda kazi. Kuona kwako, kusikia, kugusa, kunusa, ama kuonja, hatuwezi kuwa watu wa kawaida bila hizo. Kuna kasoro fulani, sehemu fulani ya maisha ambayo hatuwezi kuwasiliana nayo, bila ya hisi hiyo kutenda kazi. Nazo ni nzuri na zinatumika, na tulipewa hizo na Mungu.

53 Mungu alitupa hisi hizo, lakini zimetolewa kwako kama kipawa. Na inategemea jinsi wewe, kwamba unazifanyiza kazi kwa jambo gani, ndivyo maisha yako yatakavyoongozwa, vile unavyoruhusu hisi hizo tano. Wewe ni. . . Yale unayoona, yale unayosikia, kile unachoonja, kunusa, ama kugusa, vitu vyote vinavyoruhusiwa na hisi hizo, vitakutawala.

54 Nasi tunamshukuru Mungu ya kwamba tuna hizo hisi tano, bali kwa vyo vyote vile hukupewa hisi hizi tano zipate kukuongoza. Zilitolewa kwako kwa ajili ya mawasiliano ya

duniani. Bali ulipewa hisi ya sita, na, hisi hiyo ya sita, ni ya Mkristo peke yake. Wala huwezi kuwa na hisi hii ya sita mpaka umekuwa Mkristo; ndiyo njia pekee unayoweza kuwa na zaidi ya hisi hizo tano za kawaida kwa mtu wa kawaida. Hisi ya sita inajulikana vizuri zaidi, kwa Mkristo, kama imani. Hiyo ndiyo inayokutawala na kukuongoza, na ni ya hali ya juu kuliko hisi nyingine zote. Ni ya hali ya juu sana kuliko hisi zote, hizo hisi nyingine tano.

55 Sasa, nisingeweza kusema ya kwamba kwa sababu eti tunapokea ile hisi ya sita ya kwamba zile hisi tano hazifai tena. Naam, zinafaa. Hisi hizo tano ulipewa na Mungu, nazo zinapaswa kutumiwa. Lakini wakati hizo hisi tano zinapotenda kinyume cha Neno la Mungu, basi zinadanganya.

56 Sasa, hisi ya sita haiwezi kudanganya. Ni hisi kuu. Na hiyo ndiyo ninayotaka kunena habari zake. Asubuhi ya leo nilizungumza juu ya: *Ishara Kuu*. Na usiku wa leo juu ya: *Hisi Kuu*.

57 Na hiyo hisi kuu ni Roho Mtakatifu, ile imani ya Mungu inayokaa ndani yako. Na kama utaruhusu zile hisi tano kutii hisi ya sita, itakuongoza na kuzitiisha zile hisi nyingine zote tano chini ya hiyo hisi kuu. Kwa kuwa iko juu zaidi sana ya hisi ya kawaida, kama vile mtu wa kiroho alivyo juu ya mtu wa kawaida iko juu sana kama mbingu zilivyo juu sana, juu zaidi ya mtu wa kawaida na hisi zake tano. Inakufanya uamini vitu ambavyo huwezi kuona. Inakufanya utende ambapo hufikirii zile hisi tano zingepata kuwazia. Ibilisi anaweza kuingia katika hisi hizi tano na kukudanganya, bali hawezi kugusa hiyo hisi kuu. Hiyo iko mbali sana na anapoweza kufikia. Hiyo inatokana na Mungu. Inaitwa imani. Imani ndicho kitu hicho kikuu.

58 Basi zile hisi tano hazina mamlaka juu ya hisi ya sita, bali hisi ya sita ina mamlaka juu ya hizo hisi tano. Hisi kuu inatawala zile hisi za kawaida. Na zi—zile hisi tano ni kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Na hiyo hisi kuu ni kitu fulani kitakachokufanya uamini Neno la Mungu, kwa kuwa hilo ndilo jambo pekee itakalonena habari zake. Nayo itakufanya uamini vitu ambavyo huwezi kuona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia, maana itachukua Neno la Mungu. Nayo itakuletea Neno hilo, na kukufanya uende kinyume cha kitu kingine cho chote kilichopo ila Neno la Mungu. Kwa imani, imani hufanya jambo hilo.

59 Sasa, katika kutoa mfano huu, wa hizo hisi, mtu wa kawaida anazaliwa na hisi hizi, kwa hiyo ni hisi zinazotolewa kimaumbile. Na hilo kweli ndilo jambo pekee atakalopata kujua habari zake, katika mawazo yake ya kiakili. Yeye anaweza tu kuwazia kama mwanadamu, anaweza kuona kama mwanadamu, anaweza kufahamu kama mwanadamu, anaweza kusikia kama mwanadamu; lakini wakati anapotawaliwa, ama

kuzaliwa upya, ama tungekuita "kuzaliwa mara ya pili," basi hiyo hisi ya sita, hisi kuu inamshikilia. Na katika kufanya jambo hilo, hiyo hisi kuu inamwinua kumfikisha mahali fulani ambapo yeye ana imani ya kuamini mambo ambayo asingeweza kusikia, mambo ambayo hangeweza kuona, ufahamu asioweza kufahamu. Anaamini hata hivyo, kwa maana yeye anatawaliwa na ile hisi ya sita, ile hisi kuu. Loo, ni ajabu jinsi gani kujua jambo hilo, na kufikiria jinsi ilivyo rahisi kuliamini!

60 Sasa, huwezi kuamini mpaka uzaliwe upya. Biblia ilisema ya kwamba, "Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo, ila tu kwa Roho Mtakatifu." Tulipitia hayo juma hili lililopita. Na limekuwa jiwe la kujikwaa sana, hasa sana kwa watu wanaoamini Upentekoste, wanaponisikia nikisema jambo hilo. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Uzima wa Milele hutoka kwa Mungu, peke yake. "Wala hakuna mtu awezaye kusema Yesu ni Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu."

61 Unachukua tu yale mtu mwingine aliyosema, yale uliyojifunza kwa kisomo, yale uliyojifunza kwa hisi tano za kawaida. Lakini hisi ya sita inapoingia, Roho Mtakatifu, anaondoa hoja zote za hizi hisi sita . . . zile hisi tano, na kukuinua kukuingiza kwenye ile hisi ya sita, kukufanya uamini mambo ambayo huwezi kuona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia. Inakufanyia jambo fulani. Ndipo unaweza kusema Yesu ndiye Kristo, kwa sababu wewe umeshuhudia jambo hilo; si yale mafundisho ya kielimu yalichokufundisha, bali ni yale ambayo wewe umepitia.

62 "Hisi ya sita ni kwa ajili gani basi, Ndugu Branham? Hisi ya sita inakuja kwa sababu gani?"

63 Hisi ya sita imekuja kwa sababu hii. Sasa, hisi ya sita ni imani, hisi kuu. Sasa kama . . . Hisi ya sita imekuja kwa sababu hii pekee, hiyo ilikuwa, kufanya zile hisi tano ndani yako kukana jambo lo lote ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu. Hiyo ndiyo kazi ya hisi ya sita. Maandiko yanazungumza juu ya "kuangusha kuhojiana."

64 Zile—zile, unaona, zile hisi tano zitaninii, unaweza kuhojiana, "Vema, sasa, kwa nini mtu huyu, na kwa nini ninii . . . ?"

65 Lakini hisi ya sita haioni jambo hilo hata kidogo. Iko mbali sana na jambo hilo! Iko juu sana kuliko hiyo, mpaka hata haina hoja zo zote na jambo hilo. "Tunaliamini!" Iko mbali sana na jambo lo lote ambalo zile hisi tano zingeweza kusema juu yake. Sasa tunajitayarisha kwa ajili ya ibada ya uponyaji, unaona. "Tunaamini!" Unatembea kwa hiyo hisi ya sita, unazungumza kwa hiyo hisi ya sita, unaishi kwa hiyo hisi ya sita, unakufa kwa hiyo hisi ya sita, na kufufuka kwa hiyo hisi ya sita. Hiyo hisi kuu,

kitu fulani kilicho ndani yako, ambacho ni tofauti na alivyo mtu wa kawaida.

66 Mtu wa kawaida ana hisi hizi tu, nao wako sawa kama wanaweza kutiishwa na hisi ya sita. Kama akili ya kawaida ikisema, ikisoma Neno la Mungu na kusema, "Hilo ni Neno la Mungu," inasema Kweli. Lakini kama ikisoma, na kusema, "Lote si Neno la Mungu." Ama—ama, "Lilikuwa ni jambo fulani. Lilikuwa hivyo wakati mmoja, bali sivyo lilivyo leo." Basi hiyo hisi ya sita inaingia, na kusema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Unaona, hiyo ndiyo tofauti.

67 Hiyo ndiyo sababu watu wengi sana wanashindwa kuponywa. Wanajaribu kuja kwa wazo la kiakili. Wanasema, "Loo, mimi nina—ninafanya *hivi*, ninaamini *hili*, na kadhalika."

68 Lakini kama hiyo hisi ya sita inasema hivyo, basi hakuna kitu kitakachoweza kuwatikisa kutoka kwenye hiyo hisi ya sita. Hisi ya sita huja juu ya wanadamu kuwafanya wakane cho chote ambacho ni kinyume cha Neno la Mungu. Dalili yo yote, dalili yo yote iliyo kinyume cha ahadi ya Mungu, hisi ya sita inasema haipo, kama ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili.

69 Na muda si muda unajua, kafiri fulani, asiyeamini, anamkaribia Mkristo na kusema, "Sasa hebu angalia hapa, hakuna kitu kama huyo Roho Mtakatifu. Umekosea tu, katika jambo hilo. Una kichaa, kama unaamini upuuzi kama Huo. Hakuna kitu kama Hicho."

Hisi hiyo ya sita inaingia moja kwa moja kazini.

70 "Hebu nikuoneshe, katika Biblia, ambapo huwezi kumpokea Roho Mtakatifu. Na, unaona, ninaweza kukuonesha ambapo wanafunzi walimpokea, bali—bali . . . "

71 "Naam, vema," unasema, "angalia," hisi ya sita itakuelekeza kule na kusema, "lakini Yeye alisema, 'Ahadi hiyo ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu.'"

72 "Vema, hiyo ilimaanisha watoto wao. Hiyo, hiyo haikumaanisha ni kwa ajili yako. Si kwa ajili yako."

73 Lakini hiyo hisi ya sita inajua vizuri zaidi. Kwa nini? Iko ndani yako tayari. Wao walisema hivyo wakiwa wamechelewa sana. Umeipokea tayari.

74 Watu waliofundisha jambo hilo, "Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu," hawajui wanalosema.

75 Kama yule mvulana, wakati mmoja, aliyekuwa akimenya tofaa, naye akaulizwa na kafiri mmoja, akihoji mkutano. Akasema, "Unataka nini, unataka nini hapa?"

76 Akasema, "Ninataka kukuuliza swali." Wakati alipokuwa anakula lile tofaa na kulifurahia, mtu rahisi sana, kwa namna fulani, alionekana kama mhalifu, huku nywele zikining'inia usoni mwake, na jino moja la mbele limetokeza; na amevaa

jaketi la overoli chafu ya kale. Akasema, "Nataka kukuuliza tu swali moja."

77 Yule kafiri alikuwa ndiyo kwanza muda mfupi umepita aseme, "Hakuna kitu kama Mungu. Yote ni mhemko tu. Huo ni upuuzi, ni upuuzi tu."

78 Ndipo yule mvulana akasema, "Ninataka kukuuliza swali, bwana. Je! tofaa hili ni tamu ama ni chungu?"

Akasema, "Vema, ninajuaje? Silili."

Akasema, "Hivyo ndivyo nilivyowazia hasa," akarudi nyuma moja kwa moja.

79 Unajuaje, wakati hujamwonja Bwana? Unajuaje, wakati hujapata kumpokea Roho Mtakatifu, kama Yeye ni halisi ama kama Yeye si halisi? Unajuaje ambapo pana imani na nguvu? Unajuaje hakuna "furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu," wakati wewe hujaionja upate kuiona? Hisi ya sita inakuongoza kwenye jambo Hilo. Hisi ya sita inakutangazia jambo Hilo.

80 Hakuna nguvu za kielimu hata kidogo, zitakazoweza kukuletea jambo Hilo. Nguvu za kielimu zitahojiana na kusema, "Mbona, ni saikolojia. Ni jambo fulani *hivi*, na watu wana mhemko."

81 Lakini wakati hisi ya sita inapoingia, inakana mambo hayo yote, na kumpeleka mtu moja kwa moja hadi kifuani mwa Mungu. "Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko, na huwapa thawabu hao wamtafutao kwa bidii." Kwa imani! Kwa imani, Ibrahimu! Kwa imani, Isaka! Kwa imani, Yakobo! Yote ni kwa imani! Hisi ya sita ndiyo inayofanya jambo hilo. Hisi ya sita hukana dalili zote, dalili zote, cho chote kilicho kinyume cha Neno la Mungu, kuhisi ko kote, mhemko.

82 Mtu fulani anasema, "Loo, vema, niliombewa; bali sijisikii hata nafuu."

83 Hisi ya sita haingevumilia jambo hilo. Hisi ya sita ingesema, "Ni uongo! ninajisikia nafuu. Ninapata nafuu. Mungu alisema hivyo, hilo linamaliza kila kitu. Amina! Mungu alisema hivyo." Hisi ya sita hula Neno la Mungu tu.

84 Hiyo hisi kuu, ni kuu, ni kubwa kuliko zile hisi za kawaida. Ni hisi kuu zaidi. Ni imani. Ni nguvu inayochochea na kuendesha. Amina. Ni kitu fulani kinachokufanya utende mambo ambayo hukufikiri kamwe ungeweza kufanya. Ni hisi ya sita, hisi kuu.

85 Unaombewa. Tuseme una—una mkono uliolemaa na unaombewa, mkono wako, unakuja pale na unaamini ya kwamba Mungu atakuponya. Mchungaji anakuombea, unarudi. Maskini mtu wa kawaida atasema hivi, "Husikii tofauti yo yote katika mkono huo. Hujisikii nafuu zaidi ya vile ulivyowahi kujisikia." Bali hisi ya sita inakuja, na kusema, "Huo ni uongo! Umeombewa tayari, hilo linatosha." Amina.

86 Ni kama yule mwanamke aliyekuja kwenye mkutano wetu wakati mmoja, naye alikuwa amekuja mkutanoni, wakiwa wawili. Wakapita jukwaani. Walikuwa wameona ule utambuzi. Hao wanawake walikuwa tu—walikuwa tu wameamini kabisa. Wote wawili walikuwa ni Wakristo halisi. Mmoja akaja, na ndipo Roho akaja na kusema, "Unasumbuliwa na maumivu ya tumbo."

Ndipo uso wake ukachangamka. Akasema, "Hiyo ni kweli."

87 Ndipo Roho Mtakatifu akasema kupitia kwangu, akasema, "Na ni kidonda-tumbo. Kimesababishwa na hali ya wasiwasi. Umechunguzwa na daktari fulani, naye akasema ya kwamba usingeweza . . . ama hakina budi kuninii—ama hakina budi kufanyiwa upasuaji, kikatwe."

Akasema, "Kila neno ulilosema ni kweli!"

88 Ndipo basi alipoona yeye anaamini sana, basi akasema, "Jina lako ni Bi *Fulani*, unataka kitu *Fulani*, na mahali fulani."

Akasema, "Hiyo ni kweli!"

89 Ilikuwa ni nini? Hisi ya sita ikishika jambo hilo. Hisi ya sita pamoja na Roho Mtakatifu walikuwa wamesimama pamoja. Roho Mtakatifu alikuwa akizungumza, hisi ya sita ilikuwa ikisema "amina." Hiyo hapo. Jambo fulani halina budi kutukia.

90 Wakati Martha alipokimbilia nje kwenda kumwona Yesu, na wakati yeye aliposema, "Bwana!" Angalia hiyo hisi ya sita. "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa; bali hata sasa, lo lote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Hiyo hapo hisi ya sita.

91 Yesu alikaa kwa ujasiri, akasema, "Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa. Unayasadiki hayo?"

92 Utasemaje, hoja? Kuna mtu amelala pale, amekufa, na mabuu yanatambaa ndani yake.

93 Bali alikuwa ndiyo kwanza amalize kusema Yeye alikuwa ndiye huo Ufufuo na Uzima. Hilo ni Neno la Mungu. Hiyo hisi ya sita, imepita matibabu ya daktari, imepita mawazo ya utafiti wa sayansi. Inakataa zote, inakataa hoja zote, na kuzitupa chini. Kwa nini? Inashuhudia Neno la Mungu, "MIMI NDIMI. Mimi si 'nitakuwa, nilikuwa.' MIMI NDIMI sasa! Mimi ndimi Ufufuo na Uzima," Mwanadamu. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa. Unayasadiki haya?" Akasema.

94 "Ndiyo, Bwana," hisi ya sita, "Ninaamini kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, ambaye yuaja ulimwenguni."

"Ndugu yako atafufuka tena." Loo, jamani!

95 Haoo kaburini wakaenda moja kwa moja! Hao wawili, pamoja, ilibidi jambo fulani litukie. Hiyo ilikuwa ni hisi kuu,

huku Mungu akiwa amesimama hapo, ilibidi jambo fulani litendeke. Hisi hiyo ilikuwa ni hisi kuu, ilikuwa ni Mungu. Kulikuwa na Kitu fulani kilichokuwa kinamwambia Martha hivyo. Alikuwa amemwona Yeye. Alimjua. Alimtambua kwamba ni Masihi Mwenyewe. Na alijua, kama tu angaliweza kumfikia, kama angaliweza tu kufika karibu Naye na kumwambia kisa hicho, asikie tu ahadi moja ikitoka Kwake, hayo tu ndiyo aliyotaka. Aliposema, "Mimi ndimi huo Ufufuo na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa," hayo tu ndiyo Martha aliyotaka kusikia, ndiyo hayo tu aliyotaka.Kwa sababu, hiyo hisi ya sita, ile hisi kuu, imani yake, ilikuwa ikimsukuma kumkiri Yeye, kumwamini.

96 Mwanamke huyu, wakati alipoondoka jukwaani, ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI, "Nenda nymbani ukale. Yesu Kristo anakufanya mzima." Akaenda zake nyumbani.

97 Usiku huo, rafiki yake aliyekuwa anaishi jirani, alikuwa wa tatu ama wa nne nyuma yake, naye alikuwa na fundo kubwa shingoni mwake. Naye huyu hapa anakuja, amefurahi sana kuhusu jirani ya—yake, alikuwa ataponywa hicho kidonda tumbo kilichokuwa kimemsumbua sana. Hili lilikuwa ni moja ya mamia ya matukio, maelfu yake. Na fundo hili kubwa limetokeza shingoni mwake, naye akakaribia. Nikasema, "Hilo si jambo la mtu kutambua. Lakini unafurahishwa na jambo fulani, umefurahiwa sana, kwa sababu mwanamke yule anayeketi pale ni jirani yako." Roho Mtakatifu!

98 Akawazia, "Mtu huyo angewezaje kujua kwa jinsi yo yote jambo hilo? Lazima kuwe na Kitu Fulani kinachomfunulia jambo hilo."

99 Kwa hiyo hayo yalipotamkwa, Yeye akasema, "Unafikiria juu ya shingo yako."

"Ndiyo."

"Unaamini huo utaondoka?"

"Ninaamini," akasema, "kwa moyo wangu wote."

100 Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, nenda nyumbani na utapokea uponyaji wako."

101 Mtu wa kawaida aliangalia kote wala hakuweza kuona dalili yo yote. Mwanamke yule aliyekuwa na kidonda-tumbo akaenda nyumbani na kujaribu kula, na, jamani, nusura afe. Loo, mtu wa kawaida, hisi ya kawaida, kule kuhisi bado kulitangaza kidonda kingali kipo.

102 Kwa hiyo baada ya kama juma moja ama juma mbili kupita, alipita kwa majirani, kwa ndugu zake wote, na kanisa, akishuhudia, "Bwana ameniponya."

Nao wakasema, "Je! hivi sasa unakula?"

103 "La, si kila kitu hasa ninachotaka. Lakini," akasema, "mimi tayari nimeponywa, kwa maana kwa kupigwa Kwake nimeponywa." Haidhuru ilikuwa ni nini, alikuwa ameponywa hata hivyo.

104 Ndipo asubuhi moja, watoto walikuwa wamekwenda shuleni, naye akaona njaa sana. Alikuwa amesimama, akiosha vyombo, karibu na dirisha. Akaja mkutanoni, mkutano mwingine yapata mwaka mmoja baadaye. Naye alikuwa akiosha vyombo, na wakati yeye, jambo la kwanza, alisikia hisi ya ajabu sana ikipita mwilini mwake. Naye akawazia, "Hicho kilikuwa ni nini? Nimejisikia kana kwamba nilitaka kupiga mayowe."

105 Basi mumewe alikuwa amemwambia, kasema, "Mpenzi, acha kuzungumza juu ya kuponywa huko," kasema, "kwa maana," ingawa yeye alikuwa ni Mkristo, kasema, "unaleta aibu kwa Imani."

106 Unawezaje kusababisha fedheha wakati unaposhuhudia Neno Lake? Utasababisha shutuma usipolishuhudia.

Kasema, "Kama uliponywa, uliponywa."

107 Akasema, "Mtu huyo alisimama na kuniangalia machoni, na kuniambia shida zangu na mambo niliyokuwa nimefanya, na kwamba mimi nilikuwa ni nani, na mahali nilikotoka." Akasema, "Sikuwa nimekaa mle jengoni kwa dakika kumi na tano, wakati yeye alipokuja jukwaani. Mtu huyu angeweza kwa hali yo yote kujua jambo hilo? Sijapata kumwona maishani mwangu, naye aliniambia, "BWANA ASEMA HIVI," umeponywa." Basi huyo mama akasema, "Nitaamini jambo hilo mpaka nitakapokufa." Akasema, "Nitaamini hata iweje." Kwa hiyo yeye na dada yake aliyemfuata, rafiki fulani, walikuwa wamefanya agano kwa Mungu, ya kwamba wangeshikilia imani hiyo.

108 Asubuhi hiyo, alijihisi wa kiajabu sana, na katika dakika chache akaona njaa. Kwa hiyo watoto walikuwa wameacha shayiri katika sahani, bakuli dogo; na alisema shayiri sikuzote ilimletea uchungu tumboni. Kama mtu ye yote alipata kuwa na kidonda, mnajua ni kitu gani. Kwa hiyo akaokota shayiri hiyo na akala mego mbili tatu. Na, "Loo, jamani," akasema, "lazima nitajutia, nadhani, lakini moja ya siku hizi nitakuwa mzima." Lakini akaona angali alikuwa ana njaa, kwa hiyo akamaliza tu bakuli hilo. Akangojea dakika chache, aone kitakachotukia. Hakuna kilichotukia; akajisikia yuko mzima bado, angali ana njaa. Akajikaangia mayai machache, akamimina kikombe cha kahawa, kisha akachukua tosti chache, naye akawa na jubilii kweli kweli. Akala tu yote aliyoweza kula. Akaendelea kuosha vyombo, na yapata nusu saa baadaye, alikuwa na njaa tena. Hakuna athari.

109 Akavaa kofia yake ndogo, na huyoo akaenda moja kwa moja mitaani, akaenda nyumbani kwa kwa yule yule jirani yake.

Basi alipofika kule, akasikia, akafikiri labda kulikuwa na kilio katika familia hiyo. Walikuwa wakipiga mayowe, na kupaza sauti, na kutembea huku na huku. Mwanamke huyo alikuwa amechelewa kuamka asubuhi hiyo, basi akaamka, akitafuta ule uvimbe uliokuwa shingoni mwake, na ulikuwa umetoweka usiku huo. Ilikuwa ni nini? Mungu akitenda kazi.

110 Hapa kwenye Maskani ya Cadle, tulipokuwa na ule mkutano, yule mvulana kilema aliyekuja pale naye akaombewa. Wengi wenu mlikuwapo pale kumwona. Wakamrudisha katika chumba hicho cha dharura. Billy alinipeleka kwake. Walimleta jukwaani kwa muda wa siku tatu ama nne usiku, pale kwenye... jengoni. Hakupata kadi ya maombi, kwa hiyo wakamweka katika chumba cha dharura. Niliingia mle nikamwombea, nikamwangalia. Akasema, "Bw. Branham, unaweza kunipa faraja kidogo?"

Nikasema, "Naam, bwana, mwanangu. Polio ndiyo iliyokufanya hivi."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

111 Nikasema, "Jina lako ni *fulani*. Unatoka mahali fulani."

"Hiyo ni kweli," akasema. Akasema, "Na kuponywa kwangu je?"

Nikasema, "Kwa mapigo Yake uliponywa."

112 Akaenda nyumbani, akishuhudia, akimpa Mungu sifa. Ndipo akaleta shutuma kubwa sana, wanadai, kwa jirani, mpaka Jumapili moja kundi la wahudumu likaingia na kuketi chini karibu naye, na kusema, "Lazima uache kufanya hayo. Unasababisha lawama kwa Imani."

113 Na huyo mvulana akiwa ameketi pale, akasema, "Bwana, kama ungalikuwa umeketi mahali nilipo, kama ungekuwa kwenye kiti ninachokalia, usingejaribu kuniny'ang'anya tumaini la mwisho nililo nalo, katika Kristo." Kasema, "Kwa mapigo Yake nimeponywa." Na kabla hajamaliza kusema hivyo... Akiketi pale, amepooza miguu, mikono, mwili, mgongo. Na kabla hajamaliza kusema hivyo, huyoo akatoka kwenye kile kiti akaenda zake, akimtukuza Mungu.

114 Ni nini? Hisi zake za kawaida zilisema ataketi pale; daktari alisema atakuwa pale daima, ama mradi tu angali hai. Lakini hisi ya sita inasema, "Kwa mapigo yake mimi nimeponywa." Wala hakuwa na uhusiano wo wote na... Ni kutupilia mbali kila kitu kilicho kinyume cha yale aliyosema Mungu. Hiyo ndiyo kazi ya hisi ya sita.

115 Maskini John Rhyn, si yule R-y-a-n, R-h-y-n. Kulikuwa na mwombaji kipofu huko Fort Wayne, na kule ambako tulienda siku hiyo naye akaombewa mkutanoni. Huo ulikuwa ni usiku ule kabla ya lile piano kupiga wimbo "*Ni Tabibu wa karibu*," bila ya kupigwa na mtu ye yote akiwa karibu nayo. Na wakati

alipokuwa kipofu, alikuwa ni Mkatoliki, kwa imani. Naye—naye akasimama mstarini, nami nikamwangalia, ndipo nikasema, "Jina lako ni *fulani*, John Rhyn."

"Ndiyo."

"Wewe ni mwombaji hapo kwenye kona. Umekuwa kipofu kwa miaka mingi."

"Ndiyo, hiyo ni kweli."

"Wewe ni Mkatoliki, kwa imani."

"Hiyo ni kweli."

116 Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, pokea uponyaji wako."

Kasema, "Asante, bwana."

Nikasema, "Mshukuru Bwana."

Akasema, "Lakini siwezi kuona."

Nikasema, "Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Umeponywa."

117 Naye akasema, akaenda zake, wakamsaidia kutoka jukwaani. Mtu wa kawaida asingeweza kuona kitu cho chote. Hawangeweza kuona matokeo yo yote kutoka katika jambo hilo hata kidogo. "Mbona," wangesema, "yeye ni kipofu tu kama alivyopata kuwa hapo kabla."

118 Kwa hiyo wawili wa marafiki zake wakamrudisha na kumweka katika mstari wa maombi tena, na wakampitisha tena. Howard alimruhusu kupita. Wakati aliporudi tena, akasema, "Bwana, Wewe uliniambia niliponywa." Nikasema, "Wewe uliniambia uliniamini."

119 Akasema, "Ninakuamini. Sina sababu ya kutokukuamini." Kasema, "Umeniambia mambo yote katika maisha yangu," naye akasema, "sijui la kufanya." Kasema, "Kulikuwako na mwanamke kule nyuma akishuhudia ya kwamba alikuwa na tezi dakika chache zilizopita, na imeondoka."

120 Nikasema, "Basi kama unaniamini, mbona unanihoji? Ninakwambia Neno la Mungu."

121 Akasema, "Yanipasa nifanye nini, bwana?" Nikijua alikuwa ni Mkatoliki na ilimbidi kuwa na kitu dhahiri ambacho angeweza kushika, nilisema, "Endelea tu kushuhudia, 'Kwa mapigo yake nimepona,' na umpe sifa."

122 Maskini mzee huyo, kwa juma bili zilizofuata, ama tatu, alisimama kwenye kona na akauza magazeti, angepiga makelele, "Extra! Extra! Mungu asifiwe, nimeponywa! Extra! Extra! Mungu asifiwe, nimeponywa!"

123 Wakati aliporudi mkutanoni kesho yake usiku, ilikuwa vigumu kwangu kuhubiri, kwa ajili yake. Angesimama na kupiga makelele, "Kila mtu na anyamaze! Bwana asifiwe kwa kuniponya! Bwana asifiwe kwa kuniponya!" Akiwa

Mkatoliki, hakujua jinsi ya kushikilia imani, lakini alijua kama angeendelea kusema jambo hilo, na kuendelea, kuendelea, kuendelea, mpaka hiyo hisi ya sita ingetenda kazi. Hiyo ni kweli. "Bwana asifiwe kwa kuniponya!"

124 Alikuwa amesimama pembeni, akipaza sauti, "Bwana asifiwe kwa kuniponya! Extra! Bwana asifiwe kwa kuniponya!"

125 Angetembea huko mitaani, na hapo mtu fulani angekuja, angesema, "U hali gani, John?"

126 "Bwana asifiwe kwa kuniponya! Mimi ni mzima." Nao wakamcheka, na kumfanyia mzaha.

127 Basi maskini mvulana mwingine wa magazeti akamwongoza kwa kinyozi, akanyolewe, yapata juma nyingine mbili au tatu baadaye kutoka kwenye mkutano. Ndipo kinyozi akamketisha kitini, akampaka povu usoni. Naye akasema, "John," akasema, "Nasikia. . . " Maskini kimbelembele fulani, basi akasema, "Nasikia ya kwamba ulishuka ukaenda kumwona yule mponyaji wa Kiungu wakati" [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . hapa."

Akasema, "Naam, nilishuka kwenda huko."

128 Akasema, "Ninasikia ya kwamba uliponywa," kumfanyia tu mzaha.

129 Naye maskini yule mzee akasema, "Ndiyo, Bwana asifiwe, Yeye aliniponya," ndipo macho yake yakafunguka. Huyoo akatoka kwenye kiti cha kinyozi, na taulo shingoni; yule kinyozi akijaribu kumshika, ameshika wembe mkononi mwake. Haoo wakaenda mitaani! Kwa nini? Neno la Mungu lilianza kutenda kazi.

130 Maskini Georgie Carter akiwa yuko kule, ambaye ninyi nyote mnamjua. Baadhi ya watu wako hapa karibu. Alilala pale kwa miaka tisa na miezi minane, hakuweza hata kufanya kitu ila kuvuta kitambaa kutoka chini yake, kutoka kwenye figo na matumbo. Alikuwa na uzito wa ratili thelathini na tano hivi. Amelala kule Milltown, Indiana.

Na watu wake walikuwa wafuasi wa kanisa ambalo. . . Nilipoenda kufanya mkutano kule kwenye kanisa la Kibaptisti la Milltown, na kuwaombea wagonjwa, kanisa hilo lilisema, "Kama mfuasi ye yote wa kusanyiko hili akienda kwa huyo mshupavu wa dini, tutawatenga na kanisa." Na baba yake alikuwa ni shemasi.

131 Lakini msichana huyo alikuwa amepata kitabu changu kidogo, kinachoitwa, *Yesu Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*. Ndugu Hall alinipeleka kwake, alasiri moja. Mama yake akaikimbia mbio nyumba, asingetaka kujihusisha na jambo hilo. Niliingia nikamwombea. Kasema, "Vema, na huyo msichana wa Nale je?" Yeye alijua habari za hilo ono.

132 Nikasema, “Hilo lilikuwa ni ono, dada. Ninaweza tu kuomba. Wewe uwe na imani.” Maskini mtoto huyo alikuwa amefundishwa dhidi ya jambo hilo.

133 Siku chache baada ya hayo, nilikuwa nimesimama huko nikibatiza. Huyo msichana alikuwa huko, analia; ambapo alikuwa ameahidi ya kwamba angekuja na kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo, kama tu Mungu angemponya.

134 Na hapo, yeye, maskini miguu yake midogo kama ukubwa wa mpini wa ufagio. Wasingeweza hata kumweka kwenye karai lake la kujisaidia. Mama yake, akiwa angali kijana mwanamke, aliketi pale, anaugua kifafa, na mwenye mvi, kutokana na kumwangalia bintiye amelala pale akifa inchi baada ya inchi. Kifua kikuu cha tezi za kike, na kilienea kote mwilini. Alikuwa na uzito wa ratili kama thelathini na saba, nafikiri ndivyo ilivyokuwa, walivyokisia. Wasingeweza kumwinua juu kiasi cha kuweka karai la kujisaidia chini yake; iliwabidi kuvuta shiti la kuvutwa chini yake, la mpira. Miaka tisa na miezi minane, alikuwa amelala pale, asingeweza hata kuinua kichwa chake kuona mti uliokuwa karibu na dirisha.

135 Siku moja, nikiwa nimesimama huko msituni, huko juu kwenye mimba ya kilima, kwa George Wright, Roho Mtakatifu aliniambia, “Simama kwa miguu yako.” Ndipo nikaangalia, na kulikuwa na Nuru ikiangaza kupitia kwenye mti fulani uitwao mti-mbwa, akasema “Nenda ukapitie kwa akina Wright. . . ” Ama, “Nenda ukapitie kwa akina Carta.”

136 Nilipofika pale, Bwana Yesu alikuwa amemwonesha mama yake ishara ya kwamba nilikuwa ninakuja. Nikaingia kwa yule msichana aliyelala kwenye kile kitanda pale, mdhaifu sana hata asingeweza kuinua kikombe cha mate. Mama yake angekishikilia, anafanya “ah,” akijaribu kutema mate katika kikombe cha mate, akiwa na TB. Nikasema, “Dada Georgie. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikutana nami kule msituni, yapata nusu saa iliyopita, na akaniambia nije nikuwekee mikono. BWANA ASEMA HIVI, simama kwa miguu yako!”

137 Hisi ya sita ikaingia kazini, Nguvu fulani zikamgusa msichana huyo, kwa mara ya kwanza katika miaka mitatu. . . ama miaka tisa na—na miezi minane, alipopata kusimama, akaruka akasimama, akakimbilia viwanjani, na kubariki miti na nyasi na kila kitu, kisha akaingia na kuketi chini kwenye piano na kuanza kuimba, “*Damu imebubujika, ni ya Imanueli.*”

Kwa nini? Kuhoji kungalitupwa chini. . .

138 Asingeweza kufanya jambo hilo. Sijui sasa. Sitajua kamwe. Ni Nguvu za Mungu tu zilizomshikilia. Miguu yake haikuwa minene *hivi*, hapa juu viungoni; sijaona kitu kama hicho; ni kama vijiti. Hiyo imekuwa kama miaka ishirini iliyopita, ama kumi na minne, na leo yeye ana nguvu na afya, akimtumikia Bwana Yesu.

139 Ilikuwa ni kitu gani? Mara ya kwanza, haikuonekana kama jambo lo lote linatendeka, lakini hoja ingesema halingeweza kutukia. Lakini, ndugu, yeye alishikilia hilo Neno. Kama Mungu aliweza kumchukua msichana huyo aliyelemaa kule Salem, yule msichana wa Nale, aliyekuwa kiwete na amepooza, na mikono yake ikaning'inia namna *hiyo,* angeweza kumponya, Yeye angeweza kumponya, pia. Aliamini jambo hilo.

140 Naye Ndugu Hall, akiwa amelala kule, anakufa kwa kansa; mtu yuyo huyo aliyenichukua akanipeleka kule. Daktari wake huko Milltown alimtuma kwa daktari huyu huku New Albany, huku chini, huko ni kule kwenye Hospitali ya Mtakatifu Edwards. Ninasahau . . . Aliwalea watoto wangu; mtu mzuri, daktari mzuri. Alimchunguza, kasema, "Kansa." Akamwambia Daktari Brown, huko Milltown, kasema, "Anakufa."

Daktari Brown akasema, "Ndivyo nilivyofikiria."

141 Akamchukua akampeleka kwa dada yake chini hapa, ambaye ni jamii ya Bw. Kopp, alikuwa ni hakimu hapa mjini. Na wakati walipofika sehemu hizo, kasema, "Mweke tu hapa mpaka atakapokufa."

142 Basi wakaniagizia nishuke niende huko. Nikaenda, siku baada ya siku, pamoja na mke wangu, ndani huko. Tukamwombea Ndugu Hall. Nilimpenda. Alikuwa ni mmoja wa waongofu wangu kwa Kristo. Naye akazidi kudhoofika na kudhoofika, wala hangeweza kusogeza mikono yake.

Bibi Hall akasema, "Billy, hivi hakuna jambo unaloweza kufanya?"

143 Nikasema, "Hakuna jambo lo lote ninalojua, Dada Hall. Siwezi kusikia neno kutoka kwa Bwana. Tungeninii . . . Nikasema, "Ningetaka daktari wangu amchunguze."

Akasema, "Daktari wako ni nani?"

Nikasema, "Daktari Sam Adair."

144 Basi nikampigia simu Sam. Sam akasema, "Jambo pekee, ninaweza kumtuma Louisville, Billy, akafanyiwe eksirei na kadhalika." Kasema, "Nitakupa ripoti." Wakatuma gari la wagonjwa, kamchukua, kampeleka; likarudi.

145 Sam akanipigia simu, na kusema, "Billy, ana kansa ya ini. Hatuwezi kulikata na kulitoa ini lake, kisha aishi." Kasema, "Yeye ni mhubiri, anapaswa kuwa yuko sawa sawa sasa. Afadhali umwambie anaaga dunia."

146 Nikasema, "Yeye yuko tayari kwenda, Sam. Lakini, jambo ni kwamba, ninajisikia vibaya sana kumwona akienda. Yeye ni ndugu yangu, nami ninampenda."

Ndipo nikawazia, "Ee Mungu, nifanyie jambo fulani."

147 Nikaanza kwenda kuwinda kindi asubuhi hiyo. Nikaangalia nje kabla hakujapambazuka, hakuna mtu aliyekuwa yuko

huko uani; nikachukua bunduki yangu nikaanza kutoka ndani ya nyumba. Kulikuwa na tofaa baya lililooza likining'inia ukutani. Nikawaza, "Kwa nini Meda ameliweka hilo ukutani?" Nikaangalia, na lingine na lingine na lingine, mpaka sita yakaning'inia pale. Nilivua kofia yangu upesi na kuanguka magotini, sakafuni. Nikaangalia kule juu, ndipo tofaa kubwa mno na zuri likashuka likala yale matofaa mengine yote. Nikaangalia ikiwa imesimama kule juu, Nuru ile ile ilikuwa imesimama pale (ikining'inia kwenye *ile* picha pale) imesimama pale, ikizunguka-zunguka, kasema, "Simama kwa miguu yako. Nenda ukamwambie Bw. Hall, 'BWANA ASEMA HIVI,' hatakufa, bali ataishi."

148 Nikashuka kule na kumwambia. Hakubadilika kitu, bali aliamini jambo Hilo. Alilishikilia. Hapakuwepo na badiliko lo lote, ilivyoonekana. Siku ikapita, hakuna tofauti. Siku ya pili, hakuna tofauti. Mnamo siku ya tatu, mambo yakaanza. Naye huyu hapa anaishi leo, baada ya miaka na miaka.

149 Ninamwona akiketi hapa, Bi. Weaver. La, sijakosea. Wakati binti yake alipokuja, baada ya kuponywa kwa Magie Morgan, nilishuka nikaenda kwake wala hakukuwa na jambo lo lote ambalo mwanamke huyo angeweza kufanya. Ilikuwa afe katika masaa machache yaliyofuata. Walikuwa na sindano moja, ama mbili, walizoweza kumdunga, na hakukuwa na la zaidi. Alikuwa amefanyiwa upasuaji wa maradhi ya kike, kansa ilikuwa imeenea kwenye uti wake. Waliitawanya walipomfanyia upasuaji, wala hapakuwa na jambo la kumfanyia mwanamke huyo. Nilitaka kuzungumza naye kuhusu uponyaji.

150 Lakini akasema, "Bwana, wewe ni mhudumu wa Bwana Mungu, wala mimi sistahili uje ndani ya nyumba yangu." Akijihesabu asiyestahili kwa mhudumu kuja. Akasema, "Nimeishi maisha. Nimecheza dansi. Na nimetaka kufanya mambo ambayo sikupaswa kufanya. Nimetumia lugha mbaya, ama cho chote kile." Akaniambia dhambi zake, kisha akasema, "Mimi silistahili."

151 Nikaona alikuwa anagonga mwelekeo sahihi. Ingembidi kumwingiza Kristo *hapa* ndani kabla ya ile hisi ya sita, hisi kuu kupata kufanya kazi.

152 Tukapiga magoti. Nikazungumza naye juu ya "ingawa dhambi zako ni nyekundu sana." Akampa Bwana Yesu Kristo maisha yake. Na alipofanya hivyo, akasema, "Loo, loo, ninajisikia tofauti sana. Jambo fulani limetukia kwangu. Jambo fulani limetendeka kwangu. Ninataka kupeana mikono na ninyi nyote."

153 Na mara basi nikaangalia nje na kumwona katika ono, akirudi nyumbani akienda nyuma ya kizimba cha kuku. Nikasema, "Bibi Weaver, BWANA ASEMA HIVI, utatembelea kile kizimba cha kuku, nawe utaishi."

154 Asingeweza kufuata namna ile alivyojisikia; kansa ilikuwa imemla. Asingeweza kufuata vile daktari alivyosema; alikuwa anakufa. Na hiyo imekuwa, nadhani, miaka kumi na minne, kumi na mitano iliyopita, Bib Weaver? [Bibi Weaver anasema, "Kumi na minne."—Mh.] Kumi na minne iliyopita. Alikuja akipepesuka kwenye Maskani hii alipokuwa mgonjwa, haikuonekana kana kwamba angeweza kutoka kitandani, maskini mikono midogo iliyokonda sana; kwa maana alimwahidi Mungu angekuja na kubatizwa katika Jina la Yesu. Tulimchukua tukamtoa kwenye kiti cha wagonjwa, kwa kweli, pale kitini, tukamchukua tukampeleka kwenye kidimbwi na kumbatiza katika Jina la Yesu. Na ndiye huyo hapo ameketi, usiku wa leo. Mwangalie kama unataka kuona sampuli ya mtu mwenye afya. Kwa nini? Kutupa chini kuhojiana na utafiti wa kisayansi, na cho chote kile, kwa maana hisi ya sita ilianza kutenda kazi. Ndivyo hivyo.

155 Angalia, hebu niseme tu jambo hili tena, kwa dakika moja tu. Yesu alipita karibu na mti wakati mmoja, nao ulikuwa ni mtini. Na akauangalia huo mtini. Sasa, tafadhalini, msikose jambo hili. Akauangalia huo mtini, wala hakukuwa na tini juu yake. Ndipo akasema, akaulaani huo mti na kusema, "Mtu ye yote asile kutoka kwako."

156 Wanafunzi wakaangalia kila upande; ule mti ulionekana kama ulivyoonekana sikuzote. Saa moja tangu wakati huo, ulionekana ungali vile vile. Mungu kamwe hakufungua ardhi na kuumeza. Mungu hakutuma ndimi za umeme kutoka mbinguni na kuunguza ukawa makaa. Angeweza kufanya jambo hilo, hakika angeweza. Hakufanya mambo hayo kamwe.

157 Ilikuwaje? Ule mti ulikuwa umelaaniwa. Imani ya Mungu ilikuwa imewekwa dhidi ya uhai wa mti huo. Hakukuwa na kitu cho chote ungeweza kuona kimaumbile. Lakini huko chini kabisa chini ya ardhi, huko chini kwenye mizizi ya mti huo, kifo kilikuwa kikiingia. Ulikuwa umelaaniwa tayari. Hisi ya sita ilikuwa imekuja dhidi yake. Ulipaswa kufa. Ulianza kufa kutoka kwenye mizizi.

158 Ndio kitu kile kile kinachotendeka kwa kansa, ndilo jambo lilo hilo linalotendeka kwa uvimbe, hicho ndicho kitu kile kile kinachotendeka kwa ugonjwa wo wote wakati hisi hiyo ya sita ya nguvu za Bwana Mungu inapoinuka dhidi yake. Kasema, "Shetani toka." Huenda usione hali yo yote ya kimaumbile ikitukia mara moja hapo, lakini imani hiyo inashikilia hapo vile vile tu. Umekwisha kulaaniwa. Hiyo hisi ya sita haitaninii, hiyo hisi kuu haitaachilia. Haitaangalia unavyojisikia, jinsi wewe unavyoonekana, jinsi mtu unavyotenda. Haitahusiana kwa cho chote na jambo hilo. Neno la Mungu limetamkwa. Hisi ya sita inashikilia. Ni hivyo tu. Inaingia kazini; kansa inaanza kufifia. Inakufa kutoka kwenye mizizi, na imekufa. Hakika.

159 Kwa hisi hii hii yenye nguvu, falme zimeanguka, zikalundikana ukuta kwa ukuta.

160 Kwa hisi hii ya sita, Bahari ya Shamu ilirudi nyuma, na ardhi iliyokauka ikafanya njia kwa wana wa Mungu wapate kuepukia.

161 Kwa hisi hii hii ya sita, Samsoni aliwashinda Wafilisti elfu moja wenye ngao na mikuki. Hakuwa na njia ya kujihami, ila taya la nyumbu mwitu. Na hiyo hisi ya sita ikaanza kutenda kazi, naye akawaua Wafilisti elfu moja. Haleluya!

162 Kwa hisi hii ya sita, wafu wamefufuliwa. Kwa hisi hii ya sita, miujiza mikubwa sana imetendeka.

163 Ni nguvu yenye uwezo mkubwa sana iliyopata kuingia duniani, ni hiyo hisi kuu, inayoitwa hisi ya sita. Haina uhusiano wo wote na *hii* hapa chini; kama hii hapa chini inaitangaza na kutamka "amina", vema, unaendelea mbele; bali haidhuru hii inafanya nini, amini *Hiyo*. Hapo ndipo penye hizo nguvu, "kama unaamini moyoni mwako." Hisi yako ya tano, ya kuwazia, inakaa ndani ya ubongo wako, lakini hisi yako ya sita inakaa moyoni mwako. Unaamini kwa moyo wako. Kukiri kunafanywa kwa kwa kinywa. *Unaamini* kwa moyo wako, naam, bwana, hiyo hisi ya sita, hiyo nguvu kuu.

164 Sikilizeni, kwa sababu ya hiyo hisi ya sita, kulikuwa na nabii aliyetupwa kwenye tundu la simba. Na kwa sababu ya hiyo hisi ya sita, hao simba hawakuweza kumla Danieli. Hawakuweza. Hawakuweza kumkaribia, kwa sababu ya hiyo hisi ya sita, hiyo hisi kuu.

165 Kwa hisi hiyo hiyo ya sita, wana watatu wa Kiebrania walitupwa kwenye tanuru iliyowaka moto nao wakashinda miali ya tanuru hiyo. Hiyo hisi ya sita! Hoja zote zingethibitisha ya kwamba wangeteketea kwa moto hata wafe kabla hawajaufikia, lakini hiyo hisi ya sita iliwakinga mle ndani kwa muda wa saa mbili ama tatu. Basi walipoifungua ile tanuru, walimwona Mtu amesimama kati yao, kama Mwana wa Mungu. Hiyo ni hisi ya sita. Moto haungeweza kuichoma. Naam, bwana.

166 Ilikuwa ni hisi hiyo hiyo ya sita, wakati mmoja, ambapo Mtume Petro alikuwa amelala gerezani, nao walikuwa wanataka kumkata kichwa, kesho yake. Na huko chini katika nyumba ya Yohana Marko walikuwa na mkutano wa maombi. Hiyo hisi ya sita ikaanza kukusanyika kuzunguka jela hilo, ambapo yeye alikuwa amefunikwa na maombi. Hiyo hisi ya sita ikaanza kufanya kazi. Ile Nguzo ya Moto ikaingia dirishani na kumgusa Petro, na kusema, "Njoo huku, toka hapa." Ile hisi ya sita!

167 Ilikuwa ni hiyo hisi ya sita ambayo haingemruhusu Mtakatifu Paulo kuzamishwa kwenye ile bahari kubwa, wakati maskini meli ile ilipojaa maji. Hisi ya sita ndiyo iliyomfanya asizamishwe, ile hisi kuu. Ilikuwa ni hiyo hisi ya sita, ambayo, wakati yule nyoka alipomuuma mkononi, alimtikisia motoni. Hisi ya sita ndiyo iliyofanya jambo hilo.

168 Hiyo hisi ya sita ndiyo iliyomfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu, baada ya Yeye kulala ardhini, kwa sababu Yeye aliamini Neno la Mungu. Kasema, "Uharibuni mwili huu, nami nitaufufua tena katika siku ya tatu. Kwa maana Daudi alisema 'Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake Kuzimu.'" Ilikuwa ni hiyo hisi kuu. Tupa chini hoja za hisi *hizi*. Aminini ile hisi kuu, hisi ya imani, ambayo hutolewa na Yesu Kristo.

169 Kwa hisi hiyo hiyo, Mungu alinena wakati hakukuwako na kitu. Hiyo hisi ni nini? Hiyo hisi kuu ni Mungu, imani ya Mungu ndani yako, ile sehemu ya Mungu inayoingia ndani yako na kukupa hisi kuu. Kwa hisi kuu hiyo hiyo, Mungu aliumba ulimwengu pamoja kwa vitu visivyokuwapo wala havikutokea. Yeye alinena Neno Lake na kuamini Neno Lake, na ulimwengu ukatetema na kutokea. Utukufu!

170 Hisi ya sita, ile hisi kuu, Ee Mungu, imimine juu yangu. Nipe hiyo na kila mtu anayeihitaji. Nimiminie hisi Yako ya sita, Bwana. Niko tayari kusalimisha hizi tano, maarifa yangu mwenyewe, mawazo, kutupa chini hoja zote, Bwana. Jalia Neno Lako liwe kweli, na neno la kila mtu liwe uongo. Kila hoja, kila shaka, vitupiliwe mbali, na nijalie nitembee kwa hisi kuu, hisi ya Roho Mtakatifu.

171 Je! hutaki kitu hicho? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hicho ndicho kitu tunachotaka. Mungu akubariki, ewe rafiki. Hiyo ndiyo unayohitaji. Hiyo hisi kuu itaomba jambo fulani nayo inajua ya kwamba Yeye atalitoa. Inaamini, "Kwa maana mtu amwendeaye Mungu inambidi kuamini ya kwamba Yeye yuko, na huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii."

172 Kama hisi ya sita ikisema, "Mungu hutimiza Neno Lake. Ninajitoa Kwake. Ninasalimisha yote niliyo nayo, Kwake. Hisi yangu inasema jambo hili itatimiza hilo, imani yangu katika Neno la Mungu," kisha kuita cho chote kile, kinyume chake, kana kwamba hakikuwa.

173 Ibrahimu alikutana na Mungu, na Mungu akasema, "Utapata mtoto kwa Sara." Yeye akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye sitini na mitano. Ibrahimu aliita cho chote ambacho hakikuwapo, kilichokuwa kinyume cha jambo hilo, kana kwamba hakikuwapo. Yeye alitembea kana kwamba alikuwa amemwona Mungu, naye a—akaamini.

174 Yeye angeita cho chote kilichosema yeye hakuwa, hoja zo zote, cho chote kile ambacho. . .Huenda daktari alikuwa amesema, "Mbona, Ibrahimu, wewe ni mzee mno kuweza kufanya jambo hilo." Hilo halileti tofauti juu ya yale daktari aliyosema, yale mtu ye yote mwingine aliyosema, yale akili yake mwenyewe iliyosema, yale cho chote kile kilichosema. Mungu alikuwa wa kweli, naye alidumu nalo.

175 Hiyo ni hisi ya sita, ile hisi kuu. "Mungu, nipe hiyo. Mungu, jalia niipate zaidi," kuwahudumia watu Wake, ndilo ombi langu.

176 Asubuhi ya leo, wakati yule mama alipomleta maskini yule mtoto mchanga mwenye nywele nyekundu, akiwa amesimama hapa, machozi yakitiririka mashavuni mwake. Nikasema, "Kuna nini, dada?"

177 Akasema, "Ndugu Branham, ana kansa ya damu."

Nilisikia kitu fulani kikiibuka. Loo, "Yeye ni msaada wa utakaoonekana tele wakati wa mateso."

178 Hapa si muda mrefu uliopita, mimi na Bily tulikuwa tunashuka kwenda barabarani, tukiendesha gari. Wavulana fulani weusi walikuwa wakija barabarani nao walikuwa wakiendesha gari kwa kasi, nao walikuwa wamekwaruza gari fulani ubavuni na wakapinduka na kupinduka tena na tena, nalo likawasambaza wavulana hao barabara nzima, na maskini jamaa mmoja alikuwa amelaliwa na lile gari akiwa amelala kifudifudi. Hao wavulana wakaruka nje wakaanza kuliinua. Yeye akasema, "Jamani, tafadhalini msiliinue, mgongo wangu unavunjika! Acheni! Mtaniua! Mtaniua! Acheni kuliinua!"

179 Nao wakasema, "Loo, lazima tuliondoe juu yako, linaungua." Kasema, "Hebu . . . "

180 "Msilisogeze, mnanigandamiza karibu nife! Acheni kuliinua! Msiliinue!"

Nikampazia sauti akiwa hapo chini, "Mwanangu, je! wewe ni Mkristo?"

Akasema, "La, bwana."

Nikasema, "Afadhali uombe."

Akasema, "Naam, bwana."

181 Hisi ya sita ikaanza kutenda kazi. Nikatembea moja kwa moja kuzunguka nyuma ya lile gari, nami sitajua kamwe mpaka kwenye ile Hukumu, lakini, mara moja, gari lile lilifingirika [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.], na kuondoka juu yake, ndipo akaruka juu na alikuwa yu mzima kabisa. Ilikuwa ni nini? "Msaada utakaoonekana tele katika wakati wa mateso!"

182 Tulikuwa tunashuka kuja kutoka ninii . . . bibi mdogo mweusi alikuwa anaendesha gari barabarani, Plymouth jipya, limeisha tumika kusafiria kama maili mia nne. Alikuwa analiendesha kasi sana. Nami niliiona hilo gari. Liliingiza mtaimbo wake wa krankesi moja kwa moja kwenye mti. Mimi na Billy tukasimama. Barabara ilikuwa na theluji, inayoteleza mbele yetu, lakini wakati huo ilikuwa imekauka. Yule msichana . . . Upepo ulikuwa unavuma sana, huko Minnesota, mpaka ukalipeperusha hilo gari. Unakumbuka jambo hilo, Billy? Nikakimbilia kule kule alikokuwa. Na pale, yeye akiwa ameketi

pale, akasema, "Jamani, ninakufa mie. Nafa mie." Wakaita gari la wagonjwa.

183 Gari la wangonjwa, nao walikuwa na mtu aliyekufa amelazwa huko nyuma ya ambalanzi. Kasema, "Siwezi kumchukua."

184 Na kwa hiyo mkulima fulani akasema, "Vema, tumeni mtu mwingine, upesi, mwanamke huyu anakufa."

Nikaenda pale, na kusema, "Mama, hebu kidogo."

185 Akasema, "Jamani, usiniguse, bwana. Usiniguse. Mgongo wangu!"

186 Nikasema, "Mama, wewe ni Mkristo?" Akaniangalia. Nami nikasema, "Mimi ni mhudumu wa Injili. Kama unakufa, uhusiano wako na Mungu ukoje?"

Akasema, "Bwana, ninataka kuwa sawa, sasa hivi."

187 Ndipo hisi ya sita ikaanza ikaingia kazini. Nguvu za Mungu zikashuka. Akaweza kutembea kutoka kwenye lile gari, bila ya mtu kumsaidia. Nguvu za Mungu, zilikuwako, "Msaada utakaoonekana tele wakati wa shida."

188 Tunatembea kwa imani. Tunaishi kwa imani. "Mwenye haki ataishi kwa imani." Hatuna budi kuishi namna hiyo. Ni wangapi wangetaka kupata hiyo hisi zaidi ya sita zaidi, hisi kuu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu basi, tunapoomba.

189 Bwana wa thamani, Mungu wetu na Baba yetu, Wewe ni mwema sana kwetu. Ulitupa hisi tano kuishi kwazo na kutembea kwazo, katika dunia hii, ama ku—ama kugusa dunia kwanzo. Tunaweza kugusa vitu ambavyo—ambavyo ni vya kugusika, kwa mikono yetu, mambo yanayoshikika. Ulitupa kusikia, tupate kusikia. Tunafurahi sana kwa jambo hilo, kwamba tunaweza kusikia Neno la Mungu, na, kwa huko, "imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Tunashukuru kwa ajili ya hisi hizi sita, Bwana. Jalia tuzidumishe siku zote za maisha yetu.

190 Lakini jalia hii hisi kuu, jalia hisi ya imani, ambayo ni ya mwamini, kwa maana hana budi kuwa nayo kusudi apate kuamini. Bwana, tupe zaidi hiyo. Loo, tusafishe, Bwana, na utujaribu, na utujaze na wema Wako na nguvu Zako. Jalia tutembee siku zote za maisha yetu, kwa hisi ya sita, kwa hisi ya imani, ambayo inatolewa tu na Yesu Kristo. Ili kwamba yale tuombayo, tuweze kuamini ya kwamba tutayapokea, tusiwe na shaka moyoni mwetu, Nawe umeahidi ya kwamba yatatendeka.

191 Hawa ambao wameinua mikono yao, Bwana, ninawaombea. Walikuwa na haja. Wewe unajua zilikuwa ni nini. Ninaomba ya kwamba utazitimiza, kila moja ya hizo. Jalia jambo hilo litimie, shauku zao. Ninaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni Mmoja;
Pepo watatetemeka, na wenye dhambi wataamka;
Imani katika Yehova itatikisa cho chote kile.

192 Je! Mlipata kuusikia hapo kabla? Sasa bila ya muziki, hebu kidogo. Ba-. . .

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni mmoja;
Pepo watatetemeka, na wenye dhambi wataamka;
Imani katika Yehova itatikisa cho chote kile.

193 Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Imani ya thamani! Imani tukufu, ya thamani. Mungu, nipe imani. "Kwa imani, Ibrahimu. Kwa imani, Isaka. Kwa imani Habili alimtolea Mungu sadaka iliyo bora zaidi kuliko Kaini; yeye akiwa bado amekufa, bado alishuhudia." Jamani, jinsi tunavyohitaji imani zaidi! Ninampenda. Ninahitaji imani zaidi. Shauku yangu katika maisha haya, na kwa mwaka huu mpya unaokuja, ni imani zaidi katika Mungu. Mungu, ondoa shaka yo yote iliyo katika mawazo yangu, kama moja ikiwahi kutokea. Shetani hunipiga vita, hukupiga vita, hujaribu kututupia mishale yake. Lakini hiyo ngao ya imani ikae sikuzote mbele yangu, nikastahimili hila za ibilisi, kuzuia, kugonga mishale yake ya moto, ndilo ombi langu la moyo. Mungu awabariki.

194 Una jambo lo lote la kusema, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "La, ni kutangaza tu tena."—Mh.] Njoo huku.

*Hisi Kuu* SWA59-1227E
(A Super Sense)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 27 Desemba, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org